MAELEZO MAFUPI YA SERA

Mradi huu umefadhiliwa na Umoja wa Ulaya



Toleo la 04 | Juni 2018

# Mbinu za kukabiliana na biashara haramu ya heroini katika pwani ya Afrika Mashariki

*Simone Haysom, Peter Gastrow na Mark Shaw*

## Muhtasari

Katika miaka ya hivi karibuni, inaonekana kwamba kiwango cha heroini kilichokuwa kikisafirishwa kutoka Afganistani kupitia kwa mtandao wa njia za baharini Afrika Mashariki na Kusini kimeongezeka sana. Soko jumuishi la uhalifu linalokuza na linalokuzwa na matukio ya kisiasa katika ukanda huu, limejitokeza. Sasa hivi, Afrika inapitia kipindi cha ongezeko kubwa zaidi duniani kote la matumizi ya heroini, na aina mbalimbali za mitandao haramu na wanasiasa wa tabaka za juu wa Afrika Mashariki wamezama kabisa katika biashara hii. Sera yenye mikabala mipya inahitajika kwa dharura.

## Hoja muhimu

- Mikakati ni sharti ishughulikie changamoto hii kama mfumo haramu unaokiuka mipaka ya nchi.
- Vitendo vinavyokusudiwa kuleta mabadiliko ni sharti zielekezwe kwenye vitovu vikuu vya madawa ya kulevya vilivyo katika njia ya kusini, vikizingatia maeneo yanayoweza kuathiriwa na yale yanayoweza kuwa vyanzo vya ukosefu wa usalama, kama vile kaskazini mwa Msumbiji.
- Sharti uhusiano kati ya siasa, biashara na uhalifu wa kupangwa ufanyiwe utafiti na kushughulikiwa kikamilifu.
- Washirika wa sekta binafsi waliofanyiwa uchunguzi wanastahili kuhusishwa ili kuzuia au kuondoa uhalifu unaoenea katika bandari muhimu.
- Sharti msaada uimarishwe kwa juhudi za kijamii zitakazopunguza athari ya matumizi ya madawa ya kulevya.
- Mikakati inapaswa kupangwa ili kupunguza vurugu katika jamii za Afrika Kusini na Mashariki zilizo hatarini na zilizoathiriwa na biashara ya heroini.

Maelezo haya mafupi yanazingatia:



Tangu mwaka 2010, shehena nyingi kubwa za heroini zilizotwaliwa na Muungano wa Jeshi la Baharini – ushirika wa majeshi ya wanamaji kutoka nchi 32 wanachama yanayoendesha oparesheni za usalama wa baharini zilizo na kusudi la kukabili ugaidi na magendo ya madawa ya kulevya – zimethibitisha kwamba hivi sasa upwa wa Afrika Mashariki ni kiungo muhimu cha kijiografia katika biashara ya heroini ulimwenguni[1].

Heroini inasafirishwa kutoka Afganistani hadi pwani ya mashariki mwa Afrika kupitia njia ya baharini inayojulikana kama 'njia ya kusini'. Kwa kweli, huu ni mtandao wa njia zilizotanda Afrika Mashariki na Kusini, ambako shehena za madawa ya kulevya mwishowe hupitia zikielekezwa kwa nchi zilizo Asia, Afrika, Uropa na, kwa kiasi kidogo, Marekani Kaskazini. Katika miaka ya hivi karibuni, njia hii ya kusini imependelewa sana kwa sababu njia ya barabara ya kupitishia magendo ya madawa ya kulevya hadi mashariki mwa Ulaya kupitia nchi za Balkan imekuwa haipitiki na walanguzi hawa kutokana na migogoro na kuongezeka kwa ulinzi[2]. Hali hii imebadili baadhi ya mikondo ya kusafirisha madawa haramu ya kulevya hadi Bahari Hindi na kuendelea hadi pwani ya mashariki mwa Afrika.

Ingawa walanguzi wanaotumia njia ya kusini wanazo changamoto wanazokumbana nazo, kama vile uharamia nje ya pwani ya Somalia na oparesheni za kupambana na madawa ya kulevya za Muungano wa Jeshi la Baharini, inaonekana kwamba kiwango cha biashara katika njia hii kinaongezeka. Makadirio ya hapo awali yanaonesha kwamba tani 22 hadi 40 za heroini husafirishwa kimagendo kupitia Afrika Mashariki kila mwaka[3]. Hata hivyo, ingawa kiasi hasa kinachohusika hakiwezi kukadiriwa kwa uhakika, utafiti wetu unaonesha kwamba huenda tarakimu ziko juu zaidi.

Asasi zenye wahusika wengi na wafadhili wa kaskazini kwa kawaida wamezingatia jinsi heroini inayopitishwa kwenye njia ya kusini inavyoingizwa katika masoko ya Uropa[4]. Hata hivyo, mtazamo huu hutweza au hata kutojali athari ya biashara ya heroini katika nchi za Afrika inakopitia. Kinyume na hilo, utafiti wetu ulilenga uchumi wa kisiasa wa njia ya kusini. Utafiti huo unachunguza kwa kina sifa za usafirishaji wa heroini katika eneo hili na jinsi biashara hii ya madawa ya kulevya imezagaa katika jamii za Kenya, Tanzania, Msumbiji na Afrika Kusini.

Matokeo haya ni kilele cha utafiti wa kisayansi wa miezi minne uliojikita katika zaidi ya mahojiano 240 yaliyoendeshwa katika nchi saba. Matokeo yake kamili yamechapishwa katika makala ya utafiti ya ENACT[5]. Maelezo haya mafupi yanatoa muhtasari wa uchanganuzi huu na yanaangazia mahitimisho kadhaa hapa chini.

## Njia ya kusini na kutamba kwa uhalifu katika upwa wa mashariki mwa Afrika

Katika nchi zilizo kwenye upwa wa mashariki mwa Afrika, kuanzia Somalia hadi Afrika Kusini, biashara ya heroini imeenea sana katika jamii za maeneo hayo na inahusishwa na tabaka aali la kisiasa. Soko la heroini la Afrika Mashariki linafahamika vyema kama linalounda uchumi haramu jumuishi wa katika ukanda huu uliojikita katika heroini inayosafirishwa kutoka Afganistani kuelekea nchi za Magharibi, huku kukiwa na biashara ya kando kwa watumiaji wa eneo hilo.

> Soko la heroini la Afrika Mashariki linafahamika vyema likiorodheshwa kama sehemu ya uchumi haramu jumuishi katika eneo hili

Kupitia njia hii ya biashara ya magendo, kwanza, kiasi kikubwa cha heroini husafirishwa hadi Afrika kwa kutumia majahazi ya mbao yenye mota yaliyojengwa katika Milki za Kiarabu na kutengenezwa mahususi kwa ajili ya uvuvi. Vyombo hivi hupakiwa shehena ya bidhaa za magendo zenye uzito wa kilo 100 hadi 1,000 nje ya pwani ya Makran ya Pakistani kusini. Majahazi haya hutia nanga nje ya pwani ya Afrika katika bahari ya kimataifa, kisha mashua au boti ndogo hupokea heroini na kuipeleka kwenye fuo, ghuba ndogo au visiwa mbalimbali, au huipakua katika bandari ndogo za kibiashara. Kuna maeneo mengi kama hayo katika mwambao wote wa mashariki – kuanzia Kismayo, Somalia, hadi Angoche, Msumbiji, ambayo yanatumiwa kupakulia shehena. Njia hii hutumiwa mwaka mzima isipokuwa tu wakati wa kipindi cha miezi mitatu cha pepo za msimu katika Bahari ya Hindi (monsuni).

Ingawa kuwepo kwa biashara hii ya heroini inayotumia majahazi kumetambuliwa kwa miaka mingi, kilicho muhimu ni kwamba utafiti huu unapendekeza kwamba

walanguzi wanaopita pia wametumia kontena zilizo katika bandari nyingi zenye maji ya kina pwani. Bandari kadhaa zinadhibitiwa kwa kiasi fulani na wahalifu na zinatumiwa kuhamisha shehena ya bidhaa kadhaa haramu, kama vile pembe za tembo na mbao, kutoka kwa meli moja hadi nyingine.

Heroini nyingi inayopitia Afrika mashariki na kusini huwa inaelekea kwenye masoko ya Magharibi, ambayo yanatoa faida kubwa kuliko yale ya Kiafrika[6]. Biashara hii ya kusafirisha heroini ni biashara kubwa: ingawa wakati mwingine shehena hugawika katika mafungu madogo ili kuepuka kugunduliwa, heroini nyingi inayosafirishwa hivi hufungwa katika vifungu vya kilo kumi au hata mamia ya kilo kila kimoja. Kwa hiyo, uchumi huu wa usafirishaji hutegemea bandari na barabara za kimataifa, na, kwa kiasi kidogo sana, usafiri wa angani. Pia, biashara hii hutegemea ulinzi wa hali ya juu sana wa kisiasa, ili wale wanaohusika waweze kufaidi kwa kufikia kwa urahisi miundo msingi, kama bandari zilizo kwenye njia yao; miundo msingi iliyomuhimu sana kwa usalama wa kitaifa na inastahili kulindwa na kudhibitiwa vyema na serikali.

Mwanzoni, inaonekana kwamba ulinzi wa kisiasa uliotengewa biashara hii ulitokana na shughuli za kawaida kati ya walanguzi na wanasiasa walio na udhibiti wa bandari, forodha na utekelezaji sheria. Wafanyabiashara wa heroini wanaotumia njia hizi kusafirisha bidhaa zao wanahitaji kupanga ili bandari hizi zipitike, na pia wahakikishe kwamba bidhaa zao haramu hazikamatwi au kuhusishwa na kesi za uhalifu dhidi yao. Baada ya muda, shughuli hizi zimebadilika kwa namna mbalimbali katika upwa huu. Katika nchi ya Kenya, walanguzi wa madawa ya kulevya wameamua kugombea ofisi za kisiasa moja kwa moja. Katika nchi ya Msumbiji, walanguzi wa madawa ya kulevya wameimarisha umiliki wao wa soko kwa namna ya ajabu kutokana na fadhila wanazofanyiana kwa muda mrefu na tabaka aali la wanasiasa. Katika nchi hizi, faida inayotokana na biashara hii ya heroini hutumiwa kufadhili kampeni za wanasiasa na kulipia ulinzi wao. Hivi sasa, nchi ya Tanzania, ikiwa chini ya uongozi wa Rais Magufuli, inashuhudia mabadiliko yanayovunjilia mbali uhusiano uliopo kati ya uhalifu na siasa, na kuna ishara kwamba mabadiliko haya yamewalazimisha wahalifu kuhamia sehemu zingine za eneo hili. Nchini Afrika Kusini, heroini haijahusishwa moja kwa moja na wanasiasa, ingawa watu mashuhuri katika biashara pana ya madawa ya kulevya wamehusishwa nao.

Hata hivyo, katika njia hii ya kusafirishia heroini, si heroini yote inayosafirishwa. Kuna soko kubwa la watumiaji Afrika mashariki na kusini kuliko inavyotambuliwa. Soko hili la ndani hupata mgao wake kutoka kwa 'shehena inayovuja' kutoka kwa biashara ya usafirishaji – kupitia kwa malipo yanayotumia bidhaa hiyo yanayofanywa kwa madereva, wavuvi, polisi, na kadhalika – na pia kupitia kwa wizi mdogo mdogo unaofanywa kutoka kwa shehena kubwa. Lakini kuna ishara kwamba wahusika wakuu hupanga na kupokea shehena yao ya kibinafsi moja kwa moja kutoka Pakistani au kutoka kwa vigogo wa biashara ya kusafirisha heroini. Hususan, katika nchi ya Afrika Kusini, soko la watumiaji wa heroini ni kubwa na linazidi kupanuka, na hali hii inaendeshwa na mitandao ya ndani na ya kimataifa iliyojipanga vyema, na iliyoanzisha biashara yao ndogo ya heroini.

Kwa mujibu wa *Ripoti ya Madawa ya Kulevya Duniani ya* 2017, Afrika inashuhidia kwa hivi sasa ongezeko kubwa zaidi la matumizi ya heroini duniani, na hili limesababishwa na dhima ya Afrika katika njia ya kusini[7]. Katika nchi ya Kenya kuna takriban watu 55,000 ambao hujidunga sindano zenye heroini (mbinu ya matumizi ambayo ina hatari ya juu zaidi inayohusiana na dawa hili), zaidi ya watu 32,000 nchini Tanzania na zaidi ya 75,000 Afrika Kusini[8]. Idadi ya watu wanaovuta heroini, ambao, wengi wao wataishia kujidunga baadaye, iko juu sana. Katika nyingi za nchi hizi, kiwango cha VVU miongoni mwa watu ambao wanajidunga sindano za madawa ya kulevya kiko juu mara kadhaa kuliko ilivyo kwa wananchi wengine. Pia kuna kiwango cha juu sana cha homa ya manjano katika kikundi hiki[9].

Licha ya mwenendo wa kutia moyo ambao unahakikisha kuwa haki za watumiaji wa madawa ya kulevya na ufikiaji wao wa huduma za afya unakuwa kitovu cha mbinu za kutibu uraibu wa madawa ya kulevya katika sehemu tofauti, bado kuna mianya katika juhudi kama hizo. Kwa mujibu wa viashiria vya Shirika la Afya Duniani[10], viwango vya chanjo ya huduma ya upunguzaji wa madhara nchini Kenya na Tanzania, kwa mfano, bado viko chini. Hata Afrika Kusini na Msumbiji hazitoi chaguo za matibabu zilizojikita katika ushahidi, kama tiba ya kubadili opoiod na madawa ya kulevya, kupitia kwa mfumo wa afya ya umma. Pia kuna mianya katika ukusanyaji wa data kieneo, huku mifumo ya sheria ikiwa inayowaadhibu watumiaji wa madawa ya kulevya, na mbinu za vyombo vya usalama zikiwa ni za kikatili kwa watumiaji hao na wafanyabiashara wadogo, lakini usio na athari yoyote dhidi ya walanguzi wakuu.

Miji yenye masoko makubwa zaidi ya watumiaji – kama Mombasa, Cape Town na eneo la jiji kuu la Johannesburg-Pretoria – pia imekumbwa na vurugu inayohusishwa na biashara ya madawa ya kulevya. Kwa mfano, wakazi wa Mombasa wanasema kwamba magenge ya wahuni yameibuka katika muda wa miaka michache iliyopita ili kuwalinda vigogo wanaosimamia biashara ya heroini. Walanguzi wa madawa ya kulevya wanaajiri bila kujali kutoka kwa kundi la watu wasio ajira katika mitaa ya wachochole ya Mombasa. Nafasi za kazi zinapopungua – kama baada ya vipindi vya uchaguzi, au wakati vigogo wa wanaosimamia biashara ya madawa ya kulevya wanapofungwa – hawa 'wajasiriamali wanaotumia nguvu', tukitumia jina linalofaa, wanakuwa wanyang'anyaji na wanaingilia upokonyaji na wizi wa kimabavu katika jamii wanamoishi[11]. Wakati huo huo, na kati ya uhuru wa kutoadhibiwa uliokithiri kwa watu ambao wanapanga na kufaidi kutokana na biashara ya madawa ya kulevya, mauaji ya kiholela ya watumiaji wa madawa ya kulevya yanayofanywa na makundi ya wazalendo ya kupambana na wahalifu limekuwa jambo la kawaida.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Madawa ya Kulevya Duniani ya mwaka wa 2017, Afrika inashuhudia kwa hivi sasa ongezeko kubwa zaidi la matumizi ya heroini duniani

Pia, nchini Afrika Kusini, matumizi ya *nyaope* na *unga* yamesababisha kuongezeka kwa uhalifu, huku waraibu wakitafuta pesa za kuendelezea tabia zao kwa kuwavamia watu na kuwaibia kwa nguvu, kuiba nyaya za umeme za shaba nyekundu na shughuli nyingine haramu.[12] Hata hivyo, ni muhimu zaidi kutambua kwamba katika maeneo yanayodhibitiwa na magenge, kiwango cha vurugu kimeongezeka sana, kikiwa kinahusiana na wingi wa bunduki.[13] na vita vikali vya magenge hayo kupigania maeneo yaliyo katika udhibiti wao. Kiwango cha mauaji mjini Cape Town kiliongezeka sana kuanzia mwaka 2011 na ni hivi punde tu ambapo visa hivi vimepungua – ingawa katika viwango vya juu sana – na kuufanya mji huu kuwa mmoja kati ya miji yenye vurugu zaidi duniani, ukiwa katika kiwango sawa na miji mikuu kadhaa ya Marekani ya Kusini.[14]

Kwa hiyo, biashara ya heroini imefungamana, moja kwa moja na kwa namna isiyo ya moja kwa moja, na masuala mazito kadhaa katika eneo la Afrika mashariki na kusini. Pamoja na hayo, kuna udumishaji wa wanasiasa na vyama vya kisasa visivyo na demokrasia, dhima ya biashara hiyo katika kuzifanya bandari muhimu kutokuwa na usalama, hoteli zisizo wateja na mashamba yasiyostawishwa yanayotumiwa kama sehemu za kutakasa pesa inayotokana na madawa ya kulevya, kuenea kwa VVU na homa ya manjano, na vurugu katika jamii zinazopatikana katika maeneo ya masoko ya watumiaji wa heroini.

Maelezo mafupi ya sera huwasilisha idadi fulani ya mapendekezo, tahadhari na mawazo ya njia mwafaka ya kushughulikia biashara ya heroini kusini na mashariki mwa Afrika.[15] Muungano wa biashara ya heroini kieneo unazua changamoto kadhaa nyeti kwa juhudi za mashirika ya kiraia na walinda usalama. Hata hivyo, pia kuna fursa muhimu ya kutenda inayoweza kuchukuliwa kwa sasa.

## Mapendekezo ya sera

Hekima ya kawaida itaelekeza kwamba jibu la haraka kuhusu biashara ya heroini linapaswa kuja kwa namna ya hatua kali kutoka kwa viongozi wa kisiasa wa kitaifa na msako utakaofanywa na watekeleza sheria. Hata hivyo, mtu anahitaji kutambua shida ya asili ya kufanya kazi na taasisi za serikali zinazohusika sana katika shughuli za uhalifu wa kupangwa, isipokuwa kama kuna kikundi cha ndani kinachochochea mabadiliko.

Vivyo hivyo, hakutakuwa na faida kujenga uwezo miongoni mwa mashirika ya kutekeleza sheria kunapo ufisadi wa kina wa kimfumo – na wakati mwingine hakuna tija sana. Mara nyingi, ufaulu wa shughuli hizo hutegemea muda unaohusishwa na mwanzo wa matukio ya kisiasa. Huenda mianzo kama hiyo ikawepo Afrika Kusini katika muda usio mrefu ujao. Maafisa wa kutekeleza sheria wa Tanzania pia wameeleza, ingawa kwa njia isiyo rasmi, hamu ya ushirikiano wa kikanda, lakini bado haijabainika msimamo wa viongozi wao ni upi. Hata katika hali kama hii, sharti tahadhari kuhusu kushirikiana na vikosi vya usalama ambavyo vinachukuliwa kuwa vinakiuka haki za binadamu izingatiwe. Pia, sharti ukosefu wa mafanikio ya mikakati kama ya kijeshi kuhusu 'vita dhidi ya madawa ya kulevya' ambayo imetumiwa katika miktadha mingine, ifikiriwe. Hatimaye, kutokana na uunganishwaji wa uchumi wa pwani, uvunjaji na uondoshaji wa mitandao ya wahalifu

katika nchi moja utakuwa na athari tu ya kuwahamisha hadi kwenye maeneo ambayo hayajajiandaa kukabiliana nao.

Ingawa haya yanaweza kuonekana kama matarajio yasiyowezekana, kuna hoja kwamba hatua nzuri zaidi ya kuanza kukabiliana na changamoto hizi itakuwa ni kupata ufahamu fika wa pale ambapo juhudi zinaweza kuwa na athari kubwa kisha kubuniwe programu ambazo zinajenga ushirikiano wenye nguvu si tu kati ya watu wa tabaka aali na mashirika ya kutekeleza sheria, lakini pia watu walio katika mashirika ya kiraia.

Baadhi ya mapendekezo ya jinsi ya kutekeleza haya yamejadiliwa kwa ufupi; haya yameainishwa katika maeneo matatu:

- Kutumia mtazamo wa kikanda
- Kukabiliana na viungo kati ya uchumi wa siri na siasa
- Kujenga muungano wa mabadiliko kuhusu athari za eneo hilo

## Kutumia mtazamo wa kikanda

### Kushughulikia changamoto hizi kama mfumo haramu katika ukanda wa Afrika Mashariki

Lengo muhimu la maelezo haya mafupi ni kuonesha jinsi uchumi haramu wa pwani unavyohusisha pande mbili za mipaka ya nchi na kusisitiza haja ya kufikiri kikamilifu kuhusu suluhu. Kutokana na mtazamo wa kimaendeleo, hii ina maana kwamba tufikiri juu ya bidhaa haramu zinazovushwa mpaka kama sehemu ya mfumo unganishi wa kimaeneo – moja ikiwa na athari na matokeo yanayomilikiwa na wote. Mojawapo ya matokeo ya utafiti huu ni kwamba nchi zilizotatizwa na mfumo huu hazifikirii juu ya changamoto kwa namna hii.

Hata hivyo, inatakiwa kuwa lengo kuu la ufadhili wa maendeleo na programu za ushirika kuhimiza mtazamo kama huo wa kikanda. Kuna namna nyingi za kutoa msaada kwa mabadiliko kama hayo ya kidhana: kufadhili washauri mabingwa wa kikanda au makundi ya shinikizo ya kikanda, kusaidia kuanzishwa kwa tume ya pwani (hii ni sawa na mpango unaotumiwa sasa hivi Afrika Magharibi) na kujifunza kutokana na mchango wa nchi zote zilizoathiriwa na changamoto hii. Hoja hasa ni kutunga jibu ambalo litazingatia muungano huu na matumizi ya lugha ya mshikamano baina ya wahusika na nchi zilizoathiriwa. Kwa mantiki hii, huenda matukio ya kisiasa nchini Tanzania (na kuna uwezekano kwamba katika muda usio mrefu sana nchini Afrika Kusini pia) yakatoa nafasi mpya kwa juhudi hizo pana za kieneo za kupambana na biashara ya ulanguzi.


## Uwezo wa kushawishi wa kikanda, kwa ajili ya ukanda, pia utakuwa muhimu

Uwezo wa kushawishi wa kikanda, kwa ajili ya ukanda, pia utakuwa muhimu. Angalau serikali za nchi mbili katika ukanda huu, Msumbiji na Tanzania, hazipendi kuingiliwa na mataifa ya kimagharibi, hususan katika masuala yanayohusiana kwa karibu sana na siasa na usalama. Ikichukuliwa kwamba ushirikiano wa kikanda ni muhimu katika kushughulikia usafirishaji wa heroini katika ukanda huu, juhudi zinastahili kufanywa ili kuhimiza ushirikiano miongoni mwa nchi za ukanda huu. Kwa mfano, nchi ya Afrika Kusini ina uwezo mkubwa wa kisiasa na kiuchumi katika eneo la kusini mwa Afrika, na kwa kiasi kidogo Afrika Mashariki, na pia hasa imepata pigo kubwa kutokana na madhara ya biashara ya heroini. Kwa hiyo, huenda kuwekwa wazi kwa athari hizi nchini Afrika Kusini, na kuwezesha mazungumzo ya kikanda, kukahimiza serikali ya Afrika Kusini kushinikiza mataifa mengine ya eneo hili kushughulikia suala hilo. Lakini, ili kutimiza hili, lazima mitandao inayohusisha serikali na mashirika ya kiraia kutoka kwa nchi zilizo katika eneo hili ijengwe.

### Kujenga mitandao ya utekelezaji ya kikanda (pwani)

Mahojiano yaliyofanywa na wawakilishi wa watekeleza sheria katika sehemu mbalimbali katika pwani ya Afrika Mashariki yanaashiria kwamba mifumo rasmi ya ushirikiano wa kikanda ni dhaifu sana. Kwa mfano, maafisa wa Afrika Kusini walieleza kwamba imekuwa vigumu sana kushirikiana na wenzao kutoka Msumbiji. Licha ya matatizo haya – na ukweli kwamba aghalabu ulinzi wa kisiasa huzuia shughuli za utekelezaji sheria zenye ufanisi dhidi ya uhalifu wa kupangwa – bado inakuwa muhimu kujenga mitandao ya desturi za kitaaluma na mshikamano katika ukanda wote. Ingawa mikakati hii itabakia kuwa bwete katika baadhi ya hali hadi pale ambapo mabadiliko ya kisiasa yatakaporuhusu utekelezwaji unaofaa, huu ni uwekezaji muhimu kwa ajili ya wakati ujao.

**Maelezo jumla yanayoashiria njia za baharini na ardhini za kupitishia heroini katika mataifa ya pwani ya mashariki mwa Afrika**




*Chanzo: Shirika la Dunia la Kupambana na Uhalifu wa Kupangwa Unaokiuka Mipaka, msingi wake ukiwa mahojiano yaliyofanywa katika eneo lote, Septemba 2017*

Pia ujenzi wa mshikamano wa kikanda baina ya maafisa waaminifu huwa chanzo cha ulinzi kwa vitendo vyao. Wakati huo huo, ni muhimu kuhakikisha kwamba uhusiano mzuri unadumishwa baina ya mashirika ya kiraia na watu muhimu katika jamii ya utekelezaji sheria ya kikanda. Kusudi la kufanya hivi si kuingilia uwajibikaji wa pande hizo mbili, bali ni kutambua kwamba mashirika ya kiraia na vyombo vya habari vinaendelea kuwa kichocheo cha shughuli za utekelezaji sheria. Huu ni mtindo ulio na uwezekano wa kuendelea.

### Kulenga maeneo yanayoweza kukosa utangamano kwa urahisi

Mojawapo ya matokeo yaliyobainika katika kazi hii ni ile hali ya udhaifu iliyopo Msumbiji kaskazini. Hapa ambapo visa vinashuhudiwa kwa kiasi kikubwa bila kuangaziwa, uchumi mkubwa wa biashara ya madawa ya kulevya umekuzwa, ukiwa unawezeshwa na ufisadi na kutojali serikalini. Katika muktadha huu, kuna mengi ya kufaidi kwa kutafuta njia za kujenga uhusiano na mitandao bora, na kukusanya taarifa zaidi kuhusu uchumi wa kisiasa wa mahali hapo, ikiwa ni pamoja na namna unavyohusiana na masoko haramu.

> Uchanganuzi uliofanywa umeangazia pakubwa ukosefu wa maendeleo kuwa chanzo cha uhalifu wa kupangwa, lakini, kwa hakika, ukweli wa mambo in kinyume na hoja hii

Uchanganuzi uliofanywa umeangazia pakubwa ukosefu wa maendeleo kuwa chanzo cha uhalifu wa kupangwa, lakini, kwa hakika, ukweli wa mambo ni kinyume na hoja hii. Miundo msingi, kama vile barabara na bandari, hutoa njia halisi za kusafirisha na kushughulikia bidhaa haramu (pasipo na kanuni na utekelezaji unaofanya kazi). Kwa namna hiyo, Msumbiji kaskazini – na uwezo wake wa ukuaji wa kiuchumi unaotokana na hifadhi yake ya mafuta na gesi – iko hatarini hasa. Huku magendo ya biashara haramu ya madawa ya kulevya yakihama kutoka Tanzania kwenda kusini, sehemu hii ya eneo hili inazidi kuwa kitovu cha shughuli hii haramu. Hatua za kuzuia hali hii zinahitajika sasa ili eneo hili lisiwe chanzo kikubwa cha ukosefu wa utulivu na jukwaa la kikanda la shughuli za kihalifu Tatizo hili bado linaweza kudhibitiwa lakini hatua ya mapema inahitajika. Katika hali ya kimsingi kabisa, hatua ya kwanza ingekuwa kuongeza ushirikiano na jamii za mahali pale na kujenga mitandao yenye nguvu zaidi ya mashirika ya kiraia katika eneo hilo.

### Kutambua vitovu kisha uvifanye viwe nguzo ya mabadiliko

Katika kiwango cha juu, programu inayohusisha ukanda mzima inastahili kutambua vituo vya kijiografia, au vitovu muhimu, vitakavyozingatiwa. Vitovu ni vituo vikuu vya upokezi wa bidhaa za biashara haramu kupitia njia mbalimbali ili kuzisafirisha au kuingiza nchini, kabla ya kuboreshwa (kuchanganywa na bidhaa zingine au kuhawilisha pesa taslimu kielektroni) au kuhamishwa kutoka aina moja ya usafiri hadi nyingine (kwa mfano, kutoka majini hadi nchi kavu, au shehena za malori kuwekwa katika vifurushi vidogo kwa safari inayofuata).

Vitovu muhimu katika uchumi huu haramu wa kieneo ni Mombasa (Kenya), Nacala na Nampula (Msumbiji kaskazini), City Deep (sehemu ya Johannesburg) na Bandari ya Cape Town.

Uwekezaji unaolengwa ili kuzifanya sehemu hizi zisipitike kwa urahisi na wahalifu unaweza kufanikiwa katika maeneo mbalimbali, ukipunguza si tu usafirishwaji wa heroini, lakini pia biashara ya magendo inayohusu wanyapori au bidhaa nyingine za rasilimali asili. Hata hivyo, si lazima hatua hizi ziwe zile zinazoboresha udhibiti wa serikali au zinazoboresha utendakazi wa serikali, kwa kuwa mara nyingi maafisa maarufu wa serikali huwa wahusika wakuu katika biashara isiyo halali, na huenda udhibiti mkubwa na teknolojia bora visaidie kuendeleza biashara yao. Badala yake, kuwepo na njia bunifu za kuwawezesha wahusika halali walio na hamu ya kuiona bandari 'safi' inayofanya kazi yake ipasavyo. Kuwa na ushirikiano na mawakala wa sekta binafsi waliokwisha kuchunguzwa kwa umakini ni namna moja ya kushughulikia jambo hilo.

## Kukabiliana na uhusiano baina ya uchumi haramu na siasa

### Kuelewa athari zinazotokana na ufadhili wa vyama vya kisiasa

Ukuaji wa uchumi haramu barani Afrika, na hasa katika pwani ya mashariki, ulitokea wakati mmoja na

uanzishwaji wa demokrasia nyingi dhaifu. Pengine mojawapo ya matokeo ya kuvutia kabisa kuhusu utafiti huu ni kiwango ambacho uchumi haramu na uchumi usio rasmi na serikali zimekuwa vyanzo vya kufadhili vyama vya kisiasa katika nchi nyingi zinazohusika katika uchumi haramu unaondeshwa eneo la pwani. Ufadhili kama huo unatumiwa si tu kwa kampeni za uchaguzi baina ya vyama, lakini pia hutumiwa na watu kujipatia nyadhifa katika vyama vyao. Fedha haramu au fedha zisizojulikana na serikali zimekuwa chanzo cha 'pesa bila jasho' katika sehemu nyingi. Tokeo la moja kwa moja la hali hii limekuwa mfungamano wa maslahi ya kisiasa (na maslahi ya tabaka aali la wanasiasa) na uchumi haramu, ikiwa ni pamoja na biashara ya madawa ya kulevya.

Uchumi huu haramu una athari kubwa sana: mahojiano mengi yalizusha suala hili moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Ingawa kuna mengi yanayohitaji kueleweka kuhusu uhusiano baina ya siasa za vyama na biashara haramu, maelezo ya changamoto iliyopo yako wazi.

Mojawapo ya matokeo ya kuvutia kuhusu utafiti huu ni kiwango ambacho uchumi haramu na uchumi usio rasmi zimekuwa vyanzo vya ufadhili wa vyama vya kisiasa

Huenda si rahisi sana kuelewa athari zinazotokana na ufadhili wa vyama vya kisiasa, lakini hili ni muhimu sana katika kutenganisha shughuli halali za chama na ushawishi wa wahalifu. Jibu litahitaji kuhimiza na kuendeleza mjadala kuhusu mada hii, na kujenga miungano ya mashirika ya kiraia yenye ufanisi zaidi katika kila nchi, na hata pengine katika ukanda wote.

### Kuelewa uhusiano kati ya siasa, biashara na uhalifu

Mbinu za kisasa za maendeleo, zinazohusiana na suala la ufadhili wa vyama vya kisiasa, zimekusanya tafiti nyingi zinazoonesha thamani ya juhudi zinazoendeshwa na soko – ikiwa ni pamoja na ujasiriamali, uvumbuzi na jukumu la sekta binafsi – katika ujenzi wa ajira na upunguzaji wa umaskini. Hata hivyo kuna uelewa mdogo kuhusu jinsi msukumo wa kuwa na kundi aali la wafanyabiashara na ubinafsishaji wa makampuni ya serikali unachangia ukuaji wa uhalifu wa kupangwa barani Afrika.

Katika Afrika Mashariki, watu wanaohamahama kati ya nyanja za biashara, siasa na uhalifu hujitokeza kama walio muhimu katika kutusaidia kufahamu taasisi zinazowezesha upitaji na usafirishaji wa bidhaa haramu. Huenda kuelewa jinsi wanavyojikimu kukatoa ishara muhimu za jinsi ya kuilinda serikali kutokana na vikundi vinavyoendeleza ufisadi ndani yake. Lazima hatua zitakazochukuliwa hapa zihusishe ushirikiano na wahusika halali wa biashara, kutoa msaada kwa wanahabari za biashara (soko litakaposhindwa kufanya hivyo) na kuwafichua watu 'wanaohamahama' kwa wachunguzi wa nje.

## Kujenga miungano ya mabadiliko inayozingatia maeneo yaliyoathiriwa

### Kuelewa athari ya heroini katika mitaa ya miji ya pwani

Kote katika eneo linalochanganuliwa hapa kuna mianya katika maelezo ya kimkakati yaliyokusanywa kuhusu matumizi ya madawa ya kulevya. Uchunguzi kamili wa watumiaji wa madawa ya kulevya, bei za madawa ya kulevya na mtindo wa matumizi ya madawa ya kulevya si tu muhimu katika kuwa na mpango wa afya ya umma unaofaa kuyashughulikia, lakini pia utatoa jukwaa muhimu kwa majadiliano ya kitaifa kuhusu jukumu la biashara ya heroini katika jamii. Kwa hiyo, kuhimiza na kusaidia tafiti kuhusu madawa ya kulevya miongoni mwa jamii hizi za pwani kutakuwa muhimu katika uhamasishaji na kuchochea hatua kutoka kwa serikali.

Huenda msukumo wa sasa unaoelekeza kwa njia za kupunguza madhara katika ukanda huu ukawa mwanzo wa kujenga jitihada pana za mashirika ya kiraia. Wanaharakati na wataalamu wa afya ya umma wanaweza pia kutumia mitandao kuzua mijadala, na kuendeleza juhudi zitakazojumuisha mchango na usaidizi wa watu wanaotumia madawa ya kulevya.

### Viongozi wa jamii kama washirika

Utafiti huu umebainisha kiwango ambacho, katika sehemu nyingi, uchumi haramu umewashirikisha viongozi waliochaguliwa, kwa kiasi fulani kwa sababu

ya haja yao ya kupata pesa za kufadhili vyama vyao vya kisiasa. Hata hivyo, kote katika ukanda huu, waandishi walizungumza na viongozi wa kidini na pia wa kijamii walieolezea wasiwasi wao mkuu kuhusu athari ya matumizi ya madawa ya kulevya, hasa, kwa vijana.[16] Athari ya uraibu wa heroini kwa watu aghalabu huonekana wazi katika sehemu nyingi, huku watumiaji wachafu waliodhoofika wakionekana katika miji mingi ya pwani. Uraibu ndio unaochangia kuwepo kwa uhalifu wa ndani na huathiri maisha ya familia na jamii. Jamii zinafanya juhudi zao wenyewe huku zikipata msaada mdogo tu kutoka nje, ikiwa ni pamoja na kuanzisha kinachoitwa 'nyumba zisizo ulevi' na kuendesha kampeni dhidi ya madawa ya kulevya. Msaada (ikiwa ni pamoja na msaada wa kifedha) kwa mipango hiyo, ambayo ingebuni ujumbe wa ushirikiano katika jamii zote za pwani na kuwaelekeza viongozi wa jamii kwa desturi bora kutoka kwingineko ingekuwa njia ya kipekee na inayokuja kwa wakati unaofaa katika eneo hilo.

Ni muhimu kufundisha falsafa na mazoea ya kupunguza madhara katika juhudi za jamii kuhusu madawa ya kulevya katika hatua ya mwanzo au mapema sana. Hii ndiyo hali inayotakiwa hasa katika juhudi zinazoendeshwa na mashirika ya kidini ya sehemu hiyo, na ingawa wakati mwingine mashirika haya huwa yameelimika sana, yanaweza kuendeleza unyanyasaji ikiwa hakuna kanuni sahihi na mwongozo.

## Kupunguza vurugu zinazotokana na masoko haramu

Viwango vya vurugu vinavyohusishwa na masoko haya ya pwani hutofautiana sana. Kwa njia yoyote ile, kumulika vurugu ambayo moja kwa moja inahusishwa na uchumi haramu kutatoa njia zinazoweza kupunguza athari za mara moja, hasa kwa watu maskini na waliotengwa.

> Viwango vya vurugu vimekithiri mjini Cape Town, na jitihada chache za kuingilia kati zimefanikiwa

Kama ilivyooneshwa, labda viwango vilivyokithiri zaidi vya vurugu inayohusishwa na uchumi halifu wa pwani sasa hutokea katika sehemu yake ya kusini zaidi – huko Cape Town. Vurugu inayotokea hapa inahusishwa na matukio yanayotokea mbali kaskazini na hili litaendelea kuwa hivyo kama wingi wa walanguzi sasa kutoka Tanzania wataendelea kushiriki katika uchumi wa hapo wa madawa ya kulevya. Viwango vya vurugu vimekithiri mjini Cape Town, na kumekuwepo na jitihada chache za kuingilia kati zilizofanikiwa. Kuna chaguo nyingi za miradi inayoweza kutumiwa, mojawapo ikiwa ni kujenga mshikamano kati ya viongozi wa kijamii katika miji kama Mombasa wanaoshughulikia masuala kama hayo pwani. Kuyamulika magenge ya Cape Town pia ni muhimu ili kuondoa uhusiano wao na uchumi mpana wa kikanda na kuwalinda wakazi wa mji walio maskini na wengi walio waliotengwa.

## Kuendeleza elimu ya umma kuhusu mitandao ya uhalifu

Katika kuhitimisha, na muhimu zaidi, kuna haja ya kuwa na uelewa mpana zaidi miongoni mwa umma kuhusu hali na athari ya uhalifu wa kupangwa kusini na mashariki mwa Afrika, mbali na kuwa na uwezo wa kuutambua tu. Hapa, waandishi wa habari wanaongoza katika kufichua, kupitia kwa uchunguzi wanaofanya, uendeshwaji wa magenge ya wahalifu na uhusiano wao na siasa. Vyombo vya habari vina jukumu muhimu la kuelimisha umma kuhusu jinsi uhalifu wa kupangwa ulivyo katika nchi yao. Hili ni muhimu, kwa kuwa si rahisi kila wakati kutofautisha kati ya ufisadi na shughuli za halali za kibiashara. Kwa bahati mbaya, uandishi wa habari wa kiuchunguzi hauna ufadhili wa kutosha na waeledi wake aghalabu hawalindwi vizuri kutokana na matokeo hasi ya kazi yao nyeti.

> Vitendo vya vyombo vya habari na mashirika ya kiraia aghalabu huchangia pakubwa katika uchunguzi unaofanywa na vyombo vya usalama

Vitendo vya vyombo vya habari na mashirika ya kiraia aghalabu huchangia pakubwa katika uchunguzi unaofanywa na vyombo vya usalama, au hata, kuhusisha wanasiasa panapotokea visa vibaya vya uhalifu. Kuyapa umuhimu masuala ya uhalifu wa kupangwa – na hasa athari zake katika utoaji wa huduma, mazingira ya

mahali hapo, ukosefu wa utulivu na viwango vya vurugu – huyainua na kuyapa nafasi katika mazungumzo ya umma, ili yasipuuzwe na viongozi wa kisiasa.

## Hitimisho

Ukuaji wa biashara ya heroini katika njia ya kusini umechochewa, kwa kiasi na ukuzaji na uzalishaji wa afyuni nchini Afganistani katika kipindi cha miaka 16 iliyopita. Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, maeneo ya kukuza afyuni yalikadiriwa kuwa hekta 328,000 mwaka wa 2017, ongezeko la asilimia 63 ikilinganishwa na mwaka wa 2016. Kuna uwezekano wa ongezeko hili kubwa katika uzalishaji kuongeza usafirishaji wa heroini katika njia zote hata zaidi. Huu ni ukumbusho, ikiwa unahitajika, wa jinsi uchumi haramu duniani 'umeunganika'.

Bara la Afrika halina kinga dhidi ya madawa ya kulevya. Heroini inayopitishwa katika nchi zilizo kwenye njia ya kusini haipo katika hali ya kusafirishwa tu. Uchumi haramu wa pwani umekuwa ukikua kwa muda wa kama miongo mitatu, kupitia michakato ya uundaji wa uchumi huru, utandawazi, na mabadiliko ya kuelekea kwa demokrasia ya vyama vingi. Kwa hiyo, umeathiriwa, na kwa upande mwingine, umeathiri siasa katika eneo zima. Mji wa Mombasa ni mfano unaoonesha hatari ya kuendelea kulipuuza jambo hili zaidi. Huko, kuna walanguzi wa madawa ya kulevya waliojistarehesha sana na hata hawachunguzwi kiasi kwamba wamegombea viti vya kisiasa na kushinda. Wakati huo huo, katika maeneo ya mitaa ya vibanda ambako matumizi ya heroini ni ya juu na wakazi wanaogopa watu wanaotoa ulinzi kwa wafanyabiashara wa madawa ya kulevya na athari ya matumizi ya heroini kwa familia zao, watu wanaotumia heroini wanauawa na vikundi vya wazalendo vya kudumisha amani. Sehemu zingine, hasa katika tathmini yetu kaskazini mwa Msumbiji, zimekuwa na mazingira magumu. Kuzuia ni bora kuliko kuponya.

Ikiwa watu wenye maono ya kimaendeleo ya jinsi ya kukabiliana na biashara ya heroini hawatatoa mwongozo wa namna ya kushughulikia jambo hili, basi watu wenye misimamo mikali watafanya hivyo. Katika mkutano wa hivi karibuni ulioandaliwa na Shirika la Dunia la Kupambana na Uhalifu wa Kupangwa na Uliokiuka Mipaka, wawakilishi kutoka mashirika ya kiraia, idara za serikali na zile za utekelezaji sheria kutoka ukanda wote walikuwa na mawazo thabiti kwamba sharti mbinu zinazoimarisha demokrasia, haki za watu wanaotumia madawa ya kulevya na mahitaji ya jamii zilizoathirika vipewe kipaumbele katika juhudi hizo. Kama mapendekezo yetu hapa yanavyoonesha, wakati umefika wa kuleta pamoja wadau wote walio katika upwa wa Afrika Mashariki ili waanze kukabiliana na madhara ya biashara ya heroini.

## Maelezo


1 A Cole, Heroine trafficking in the Indian Ocean: Trends and responses, Galle Dialogue, 1–2 Desember 2014.

2 Ofisi ya Umoja wa Mataifa kuhusu Madawa ya Kulevya, *Ripoti ya UNODC kuhusu madawa ya kulevya ya 2015*, Vienna: UNODC, 2015, Dibaji; UNODC, Biashara ya opiate ya Afghan kupitia Njia ya Kusini, Vienna: UNODC, 2015.

3 J Wright, Transnational organized crime in Eastern Africa: A threat assessment, Vienna: UNODC, 2013.

4 Heroini inayopitia njia hii pia husafirishwa hadi nchi nyingine, ikiwa ni pamoja na masoko ya Asia na baadhi ya mataifa ya visiwa vya Bahari Hindi.

5 Watafiti sita waliteuliwa kufanya utafiti kati ya Julai na Agosti 2017. Baadaye kikundi cha wataalamu kutoka nje kilitembelea miji na majiji kadhaa katika maeneo yale yale kwa wiki tatu mnamo Septemba 2017, kuthibitisha na kupanga taarifa kulingana na vyanzo vya awali vilivyorejelewa, pamoja na kufanya mahojiano zaidi. Kikundi hiki cha wataalamu kilifanya safari kadhaa na pia kupiga simu ili kutathmini kazi ya watafiti wenyeji na kufuatilia idadi fulani ya wahojiwa. Mbali na mahojiano katika nchi za msingi za uchambuzi – Kenya, Tanzania, Msumbiji na Afrika Kusini – mahojiano mengine yalifanywa Ushelisheli na Pakistani miezi ya Oktoba na Nowember 2017 ili kupata ufahamu bora wa njia zinazoingia Afrika, na karibu mahojiano 50 yalifanywa nchini Uganda katika juhudi za kuelewa uhusiano wa ndani. Tazama ripoti yetu kamili kwa maelezo zaidi.

6 Uchumi wa hali hii ni dhahiri: nchini Pakistani, gramu ya heroini inagharimu takriban dola 3 za Marekani na nchini Kenya ni takriban dola 20 za Marekani, ilhali kule Uingereza inagharimu dola 61 za Marekani na nchini Denmark ni dola 213 za Marekani. Tazama bei ya madawa ya kulevya kama ilivyoorodheshwa katika Hovoscope.com. Bei hizi ni za tarehe 16 Novemba 2017.

7 UNODC, *World drug report 2017* booklet 3, Vienna: UNODC, 2017.

8 Taarifa zilizotolewa na nchi husika kwa UNODC kulingana na mahitaji ya kuripoti ya Hojaji ya Ripoti ya Mwaka kwa Ripoti ya Dawa ya Dunia.

9 Nchi kadhaa za Afrika Mashariki zimeonesha uongozi wa kimaendeleo katika juhudi zao za afya ya umma kuhusu matumizi ya madawa ya kulevya kwa kudunga sindano. Wote kutoka Kenya na Tanzania (ikiwa ni pamoja na Zanzibar) wameupa umuhimu upunguzaji wa madhara katika majibu yao.

10 S Larney et al, Global, regional, and country-level coverage of interventions to prevent and manage HIV and hepatitis C among people who inject drugs: A systematic review, *The Lancet*, 5:12, 2017, e1208–e1220.

11 Jambo hili lilibainishwa na wahojiwa walio na uzoefu wa moja kwa moja wa mashambulizi hayo katika mkutano wetu wa kikundi cha wataalamu huko Nairobi tarehe 13 Novemba 2017. Angalia pia M Schuberth, The impact of drug trafficking on informal security actors in Kenya, *Africa Spectrum*, 49:3, 2014, 55–81.

12 *Nyaope* ni mchanganyiko wa madawa mbalimbali na viungo vingine ulioenea Afrika Kusini; *unga* ni madawa ya kulevya yenye heroini yaliyo na uraibu mkubwa.

13 Imeripotiwa kwamba bunduki zimechukuliwa kinyume cha sheria kutoka kwenye maghala ya silaha ya polisi huko Western Cape na kuuziwa majambazi tangu 2010. Angalia C Dolley, polisi wa Western Cape na mfanyabiashara anayeuza bunduki washikwa katika uchunguzi mkubwa wa silaha, News24,10 Oktoba, 2017, https://www.news24.com/SouthAfrica/News/western-cape-cop-gun-dealer-arrested-in-massivew firearms-probe-20171010.

14 Takwimu za hivi karibuni za mwaka 2016/17 zinaonesha vifo 63 kwa kila wananchi 100,000 – linganisha hilo na vifo 42 kwa kila wananchi 100,000 katika mwaka 2009/10. Takwimu za Cape Town ni maradufu jumla ya kitaifa. Data hii imetoka Taasisi ya Utawala wa Usalama na Masomo ya Uhalifu katika Chuo Kikuu cha Cape Town. Inatoa data yake kutoka Huduma ya Polisi ya Afrika Kusini lakini kwa kuwa mipaka ya mji haipatani na ile ya polisi, inabidi ikokotolewe upya.

15 Na, kwa kweli zaidi ya hivyo: nchi nyingine nyingi zilizo katika njia ya kusini zimeathiriwa pia na mienendo hii.

16 Wakati wa kumtembelea kiongozi mmoja wa dini, kwa mfano, tumekuta chumba chake cha kusubiri kimejaa wenyeji waliokuwa wanatafuta msaada kwa ajili ya jamaa wao waliokuwa wamenaswa na uraibu wa heroini ya bei ya chini.

Mradi huu umefadhiliwa na Umoja wa Ulaya



## Kuhusu waandishi

Mark Shaw ndiye mkurugenzi wa Shirika la Dunia la Kupambana na Uhalifu wa Kupangwa Unaokiuka Mipaka ya Nchi (GIATOC) na pia ni mwanazuoni mwandamizi katika Mradi wa Kimataifa kuhusu Sera ya Madawa ya Kulevya katika Shule ya London ya Uchumi. Mpaka hivi karibuni amekuwa Profesa wa Haki na Usalama katika Kituo cha Elimu ya Jinai katika Chuo Kikuu cha Cape Town, anakofundisha. Amewahi kufanya kazi katika nyadhifa mbalimbali katika Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayohusika na Madawa ya Kulevya na Uhalifu.

Peter Gastrow ni mshauri mkuu wa GIATOC. Anaishi Cape Town na amefanya kazi kama wakili wa Mahakama ya Upeo, ameshahudumu kama mbunge, na pia kama mshauri wa waziri wa polisi wa Afrika Kusini. Uhalifu wa kupangwa umekuwa swala analolizingatia katika utafiti wake tangu afanye kazi kama mkurugenzi wa Cape Town wa Taasisi ya Masomo ya Usalama, na mwanazuoni mwandamizi katika Taasisi ya Kimataifa ya Amani huko New York.

Simone Haysom ni mchanganuzi mwandamizi wa GIATOC na pia ni mwanazuoni anayetembelea Idara ya Masomo ya Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Oxford. Amewahi kufanya kazi kama mtafiti katika Taasisi ya Maendeleo ya Ng'ambo ya London, na amefanya kazi miaka mingi kama mtaalamu wa masuala yanayohusiana na uhamishwaji wa lazima kutoka kwa makazi, maendeleo ya miji, uhalifu wa kupangwa na kazi ya polisi.

## Kuhusu ENACT

ENACT hujenga maarifa na ujuzi ili kuboresha namna Afrika inavyoshughulikia uhalifu wa kupangwa unaokiuka mipaka ya nchi. ENACT huchanganua jinsi uhalifu wa kupangwa unaathiri uthabiti, uongozi, utawala wa sheria na maendeleo barani Afrika, na hufanya kazi kupunguza athari zake.

ENACT hutekelezwa na Taasisi ya Masomo ya Usalama (Institute for Security Studies, ISS) na Shirika la Polisi Ulimwenguni, INTERPOL, wakishirikiana na Shirika la Dunia la Kupambana na Uhalifu wa Kupangwa Unaokiuka Mipaka ya Nchi (Global Initiative against Transnational Organised Crime, GIATOC).

## Shukrani

ENACT imefadhiliwa na Umoja wa Ulaya. Chapisho hili limetolewa kwa usaidizi wa Umoja wa Ulaya.

ISS INSTITUTE FOR SECURITY STUDIES

INTERPOL

THE GLOBAL INITIATIVE AGAINST TRANSNATIONAL ORGANIZED CRIME

Picha ya jalada: © Africa Studio – Adobe Stock

Yaliyomo katika chapisho hili ni mali ya mwandishi pekee na hayawezi kwa namna yoyote ile kuchukuliwa kuwakilisha maoni au msimamo wa Umoja wa Ulaya, au ushirikiano wake na ENACT. Waandishi huchangia machapisho ya ENACT kama watu binafsi.

© 2018, ENACT. Haki ya kunakili ya juzuu hili imepewa ENACT, washirika wake, Umoja wa Ulaya na mwandishi, na hakuna sehemu yoyote inaweza kutolewa tena kikamilifu au katika sehemu bila ruhusa ya moja kwa moja, kwa maandishi, ya mwandishi na ushirikiano wa ENACT.